JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## WITO WA KUSHIRIKI KATIKA TUZO ZA WSIS, PICHA BORA NA UWASILISHAJI WA MIRADI YA TEHAMA KWA MWAKA 2026

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kwa kushirikiana na Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya Habari (WSIS) na waratibu wake, linawaalika wadau wote kuchangia katika uwasilishaji wa miradi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye kanzidata ya WSIS na kushiriki tuzo za WSIS 2026. Miradi hii inabidi iwe yenye kulenga kuhamasisha teknolojia bora za habari na mawasiliano kulingana na mpango-kazi wa WSIS na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea: **www.wsis.org/stocktaking** na **www.itu.int/net4/wsis/stocktaking/Prizes/Prizes/**.

Aidha, Shindano la Picha la WSIS, linalofanyika kila mwaka, limefunguliwa kwa washiriki wote. WSIS inawakaribisha washiriki kuwasilisha picha zinazoonesha jinsi TEHAMA inavyochangia katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Washindi watatu wa Shindano hili la Picha watapokea zawadi wakati wa Mkutano wa Jukwaa la hadhi ya juu la WSIS 2026. Kwa maelezo zaidi fuata: **www.itu.int/net4/wsis/forum/2026/PhotoContest**.

TCRA inawaomba wadau wote, zikiwemo taasisi za Serikali, sekta binafsi, taasisi za kimataifa na kikanda, asasi za kiraia na wanataaluma, kutumia fursa hii na kuwasilisha miradi au mipango inayoutumia uwezo ya TEHAMA kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Hairuhusiwi taasisi moja kuwasilisha zaidi ya mradi mmoja kwa kila kipengele. Wadau wanahimizwa kusoma na kuzingatia kanuni za uwasilishaji wa mradi na vigezo vya ushiriki vinavyopatikana kwenye tovuti ya tuzo za WSIS. Wadau wote wa WSIS wanahimizwa kuwasilisha miradi ya TEHAMA ambayo wanaamini inakidhi vigezo vya kutambuliwa na kukuzwa, ikiwemo miradi iliyo na isiyo chini ya umiliki wao.

Orodha ya miradi iliyochaguliwa itatangazwa tarehe **11 Aprili 2026**. Wadau wa WSIS watashiriki kuipigia kura tarehe **30 Aprili 2026**.

Miradi Kumi na Nane (18) itakayoshinda itatangazwa pamoja na miradi mingine **72** katika sherehe ya tuzo za WSIS 2026 kwenye tukio la mkutano wa kilele wa **www.itu.int/net4/wsis/forum/2026/en** WSIS 2026 utakaofanyika tarehe **6 Julai 2026**. Miradi iliyoshinda itaoneshwa kwenye machapisho ya WSIS katika kipengele cha Mafanikio, aidha maelezo ya shughuli zote za mradi na shughuli zake yatachapishwa katika Ripoti ya Miradi ya WSIS 2026.

Ukomo wa uwasilishaji wa miradi kwenye tuzo za WSIS ni tarehe **15 Machi 2026** na shindano la Picha la WSIS ni tarehe **20 Machi 2026**.

Imetolewa tarehe **5 Februari 2026.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Thu Feb 05 14:39:32 EAT 2026

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz